# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

## Awamu ya 2 Mwaka wa 2

# 94 Sauli anageuka

### Kwa Biblia

Matendo ya Mitume mlango wa 9 : 1 – 25

### Kiini cha somo

Kuonyesha vile Mungu aliita Sauli amfuate na ahubiri Injili kwa Mataifa.

### Somo

Wakuu wa Wayahudi na Wayahudi wengine kwa jumla hawakupenda Wakristo. Wayahudi wa Yerusalemu walikuwa wanazuia watu wasihubiri juu ya Yesu. Wakristo wengi waliteswa. Baadhi yao walifungwa gerezani na wengine kuawa. Baadhi yao walitoroka kutoka Yerusalemu. Walienda kuishi kwa miji mingine. Walihubiri Injili popote walienda. Hata hivyo kulikuwa na Wakristo kwa miji mingine. Hii iliwakasirisha Wayahudi sana.

Sauli alikuwa Myahudi. Alikuja Yerusalemu kujifunza sheria za Wayahudi. Sauli alichukia Wakristo sana. Aliwatupa wengi gerezani hapo Yerusalemu. Sauli aliona vibaya sana aliposikia kwamba Wakristo wameenda kuishi kwa mji wa Dameski. Wakristo walikuwa wamehubiri Injili Dameski. Kule kulikuwa na kanisa la nguvu la Kikristo.

Sauli alienda kwa Kuhani Mkuu. Aliomba apewe barua ili apelike Dameski. Hizo barua zilipea Sauli ruhusa ya kuwashika Wakristo. Alitaka ashike Wakristo wote, waume kwa wake. Angewaleta Yerusalemu ili watupwe gerezani.


## Maswali

1. Nani alichukia Wakristo?
2. Mbona Sauli likuwa anaenda Dameski?
3. Nini ilifanyika njiani alipokuwa akienda Dameski?
4. Nini ilikuwa mbaya na Sauli aliposimama juu?
5. Sauli alifanya nini kwa siku tatu? Hangeweza kufanya nini?
6. Yesu aliambia Anania afanye nini?
7. Mbona Anania hakutaka kwende kuona Sauli?
8. Yesu aliambia Sauli nini kuhusu Sauli?
9. Vitu 3 gani vilifanyika kwa Sauli alipokutana na Anania?
10. Sauli aliheba kutoka Dameski namna gani?

## Majibu

1. Wakuu wa Wayaudi, Wayahudi na Sauli hawakupenda Wakristo.
2. Kuwashika Wakristo na awalete Yerusalemu gerezani.
3. Mwangaza mkuu ulimlika. Yesu alimuuliza mbona alikuwa anamuudhi. Yesu aliambia Sauli aende Dameski.
4. Sauli alikuwa kipofu.
5. Sauli aliomba msamaha. Hakukula wala kukunywa.
6. Yesu aliambia Anania aende amponye Sauli.
7. Anania alijua kwamba Sauli alikuwa akitesa Wakristo.
8. Yesu alimwambia kwamba alikuwa amemchagua Sauli aende ahubirie Mataifa.
9. Alipata kuona. Alipata Roho Mtakatifu. Alibatizwa.
10. Wakristo walimweka kwa kikapu na kumteremshia kwa ukuta nje ya mji.

Safari ya kuenda Dameski ilikuwa ndefu. Lakini mwishowe Sauli alikaribia Dameski. Bunde tu mwangaza mwingi uliangazia Sauli. Sauli alifunika macho yake na akaanguka chini. Sauli alisikia sauti ikisema, Sauli,Sauli, mbona unaniudhi? Sauli alishangaa. Akauliza, “Wewe nani Bwana?” Yesu alijibu, “Mimi ni Yesu, unayemuudhi.”



Yesu alimwambia Sauli ainuke na aende mpaka Dameski. Kule ataambiwa afanye nini.

Watu wote waliokuwa wakisafiri na Sauli walishangaa. Wangesikia sauti lakini hawakuona mtu yeyote. Kulikuwa na mwangaza ulioangaza kuliko mwangaza wa adhuhuri. Sauli aliposimama alijipata ako kipofu. Wenzake walimsaidia mpaka Dameski.

Sauli alikaa Dameski kwa siku tatu bila kukula wala kunywa. Aliomba Mungu akitaka amsamehe. Hakukuwa ameamini Yesu. Alikuwa ametesa Wakristo waliofuata Yesu. Sauli aliaibika sana. Aliuliza Mungu amsamehe.

Anania alikuwa Mkristo. Aliishi Dameski. Anania alikuwa na ndoto. Kwa ndoto, Yesu alimwiita, “Anania.” Anania alijibu, “Hapa Bwana.” Yesu alimwambia, “Enenda kwa Barabara Nyofu kwa nyumba ya Yuda. Uliza mtu aitwae Sauli. Sauli ako anaomba nimsaidie. Enenda umponye apate kuona.”

Anania hakutaka kwenda. Aliambia Yesu, “Bwana, Sauli ni mtu mwenye ako anatesa Wakristo. Amekuja hapa kuwashika Wakristo. Atawapeleka Yerusalemu kuwafunga gerezani.” Lakini Yesu alimjibu, “Enenda kwa sababu nimemchagua ahubiri injili kwa Mataifa.”

Anania alienda kwa Barabara Nyofu kwa nyumba alikokuwa Sauli. Anania aliambia Sauli, “Ndugu Sauli, Bwana Yesu aliyekuonekania kwa barabara ukienda Dameski, amenituma nikuponye macho. Huyu Yesu atakupa nguvu za Roho Mtakatifu.” Bunde tu, vitu kama magamba zilianguka kutoka kwa macho ya Sauli. Akaanza kuona tena. Papo hapo, Sauli alibatizwa.

Sauli alikaa Dameski na Wakristo wenzake. Sauli alifundisha watu juu ya Yesu na Ufalme wa Mungu. Wakuu wa Wayahudi na Wayahudi wa Dameski walikasirika sana.Sauli alikuwa amekuja Dameski kuwashika Wakristo na awafunge. Badala yake alikuwa amekuwa Mkristo. Alikuwa anafundisha watu juu ya Yesu.

Wayahudi walipanga kuua Sauli. Kulikuwa na ukuta uliozunguka mji wa Dameski wote. Kila mtu alienda nje na ndani ya mji kupitia kwa milango. Wayahudi walilinda kwa milango. Walipanga kuua Sauli alipokuwa akitoka kupitia kwa mlango.



Wakristo walisikia juu ya huu mpango. Usiku ulipoingia, walificha Sauli ndani ya kikapu. Walisukuma hicho kikapu kupitia kwa tundu ya ukuta. Waliteremsha kikapu mpaka chini nje ya ukuta. Sauli aliheba kutoka Dameski. Wakristo kwa muda mfupi, walipumzika kutoka kwa mateso.